

**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA  
TAREHE 18/11/2021.**

**MAHUDHURIO**

**A1: WAJUMBE**

|    |                        |                              |        |
|----|------------------------|------------------------------|--------|
| 1. | Bw: Samwel Oberlin     | Idara ya Mazingira           | M/kiti |
| 2. | Bw: Malick Panja       | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi | Katibu |
| 3. | Bi: Mary Kambaine      | Idara ya Maendeleo ya Jamii  | Mjumbe |
| 4. | Bw: Bazilio Mwanakatwe | Idara ya Utawala             | Mjumbe |
| 5. | Bw: Philemon Chaula    | Idara ya Ardhi na Maliasili  | Mjumbe |

**A2: WASIOHUDHURIA**

|    |                   |   |         |
|----|-------------------|---|---------|
| 1. | Adv: Peter Salama | Mkuu wa Kitengo cha Sheria<br>(kwa taarifa) | Mshauri |
|----|-------------------|---|---------|

**C: SEKRETARIETI**

|    |                    |                                    |
|----|--------------------|------------------------------------|
| 1. | Bw: Fredrick Kweka | Mwandisha wa Vikao vya Halmashauri |
|----|--------------------|------------------------------------|

**Agenda za kikao**

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuridhia agenda
3. Maombi ya Idhini ya kupitisha Miradi ya "UVIKO 19"
4. Kufunga Kikao

**AGENDA NA 1. KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwasalimu Wajumbe na kuwakaribisha katika kikao. Alieleza kuwa kikao hicho ni cha dharula. Baada ya hapo katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe na kuwakaribisha katika kikao. Alieleza kuwa suala kubwa ni kujadili kwa kina juu ya agenda iliyopo mbele yetu na ameomba ushiriki mzuri wa wajumbe. Baada ya hapo mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 07:10 Mchana.

**AGENDA NA 2. KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe walipitia agenda zilizowasilishwa na kuridhia kujadiliwa.

**AGENDA NA 3. MAOMBI YA IDHINI YA KUPITISHA MIRADI YA "UVIKO 19" KWA NJIA YA "FORCE ACCOUNT"**

Katibu aliwasilisha taarifa hiyo ambapo alieleza kuwa Halmashauri imepokea fedha jumla ya Tsh 623,600,000.00 kutoka serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mbalimbali iliyoelekezwa katika Shule za msingi, Shule za sekondari Pamoja na Afya, kwa mchanganuo ufuatao;

- i) Idara ya Elimu Msingi – Tsh 132,800,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum na ujenzi wa Vyoo matundu 12 kila shule katika shule nne (4)
- ii) Idara ya Elimu Sekondari – Tsh 400,800,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba za madarasa 24 katika shule 11 na ujenzi wa matundu ya vyoo 12 kila shule katika shule mbili (2)
- iii) Idara ya Afya – Tsh 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi (3 in 1) katika Hospitali ya Wilaya ambapo maelekezo ya TAMISEMI yameitaka Halmashauri kutumia njia ya Mkandarsi au “Force Account”

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Wajumbe walihoji kama fedha hizi zipo katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022.? Katibu alijibu kuwa fedha hizi hazipo katika mpango wa manunuzi zimekuja nje ya bajeti hivyo tunatakiwa kuziombea vifungu vya malipo kwa ajili ya utekelezaji.


Wajumbe walitaka kujua majina ya shule hizo na Katibu alizitaja kama ifuatavyo:  
Elimu Msingi: S/M Lupata (Mahitaji Maalum), S/M Malema, S/M Bwilando, S/M Ngululwale na S/M Manow.

Elimu Sekondari: Busokelo Boys, Mwakaleli Sec, Isange Sec, Kabula Sec, Ndembo Sec, Mzalendo Sec, Selya Sec, Kifunda Sec, Lufilyo Sec, Ikapu Sec na Ntaba Sec.

Wajumbe walipokea na kuridhika na majibu hayo, na kwa pamoja waliridhia utekelezaji wa kazi za ujenzi katika Shule za Msingi na Sekondari tajwa itumike njia ya “force account” pekee isipokuwa katika ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika Hospitali ya Wilaya itumike njia ya Mkandarasi au ‘force account’ baada ya tathimini halisi ya gharama kufanyika. Hata hivyo bodi imeshauri mchakato wa kutafuta mafundi na ununuzi wa vifaa uanze mapema na kuletwa kwenye vikao vya bodi kwa ajili ya kupata idhini.

#### **AGENDA NA 4. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kujadili kikamilifu agenda zilizowasilishwa na alifunga kikao saa 08:16 mchana

  
.....

**BW: MALICK PANJA**

**KATIBU**

**UMETHIBITISHWA NA**

  
.....

**SAMWEL OBERLIN**

**MWENYEKITI**

**TAREHE.....** 07/12/2021